Teacher.co.ke

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
# KISWAHILI 102/2
# MUHULA WA PILI 2026
## UFAHAMU

a) i) Ufisadi
ii) Uongozi mbaya
iii)Turathi za kikoloni
iv) Uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika
v) Idadi kubwa ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi taifa linalohusika
vi) Ukosefu wa nyenzo na mali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini
vii) Ukosefu wa elimu na nafasi za ajira (4x1=4)

b) Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. (2x1=2)

c) i) Kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini
ii) Pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni masikini
iii) Kuzalisha nafasi za kazi kwa dharura
iv) Kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi
v) Kuendeleza elimu
vi) Kuimarisha miundo msingi (1x4=4)

d) Ni chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umasikini zaidi (1x2=2)

e) i)kulitadarukia – kulishughulikia, kulitatua kulikabili
ii) Kuatika - kuanzisha , kutia , kuzua
iii) Kuyaburia madeni. Kuyasamehe madeni, kuyaondolea madeni (3x1=3)

**2. MUHTASARI**

(a) (i) Katika nchi zilizoendelea, vijana wanapokamilisha masomo hujawa na mawazo mengi ya kazi watakazozifanya.
(ii) Hawana uhakika ni kazi zipi watapenda kuzifanya.
(iii) Hufikiri na kubadili nia kuhusu jambo hili.
(iv) Wakuapo kimwili na kiakili hufikiria kazi moja itakayowafaa na iliyo karibu na kwao.
(v) Baadaye hukata shauri kufanya kazi moja maalumu.
(vi) Hufikiria uamuzi huo wagunduapo kuwa kazi watakazofanya zinategemea elimu na akili walizo nazo. wa
(vii) Wanapoanza kufanya kazi hugundua maisha ni tofauti
(viii) Wasimazi wao ni tofauti na walimu

(7x1 = 7)

(b) (i)Hugudua maisha ni tofauti na ya awali
(ii)Hugundua kuwa wasimamizi wao ni watu tofauti kabisa na walimu wao wa shule.
(iii) Hawa hutaka kazi zifanywe bila uvivu / uzembe.
iv)Hawa si wavumilivu kwao.
v)wanapomaliza shule hufanya kazi kama za wazazi wao
vi)Hufahamu kuwa hakuna kazi rahisi.
vii)Siku yao ya kwanza kazini hujiona wako katika hali ya ukiwa.

viii)huwa na hatari ya kuondolewa kazini au kazi yenyewe kufungwa. (6 x 1 = 6)


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

M a – 7
b – 6
ut - 2

MATUMIZI YA LUGHA

a) i) /g/
ii) /sh/

b pendo

c tengwa /jengwa/ bingwa/ mbwa aonyeshe /abainishe kitahini

d) – kiambishi awali cha vitenzi jina – kuimba
- Upatanisho wa kisarufi – kujitolea kwao kunaudhiu
- Kiambishi cha mahali - kule / huku
- Kijalizo cha vitenzi vya silabi moja – ku-nywa /ku –fa
- Kikanushi cha wakati uliopita.
(**Aonyeshe mifano)**

e) i) Ukwenzi / mkwenzi / ukweaji / kukwea
ii)upinde / pindo / upindo/kupinda

f) Sijamchoresha/ hakiki majibu ya mwanafunzi

g) i) Kufungia maneno - AKA! (Huonyesha ghadhabu)
ii) Kufungia herufi/nambari (i) (a)
iii)Hufungia maelekezo/maelezo kwenye mazungumzo
Tatu: (Akibisha mlango)
Mwanafunzi aonyeshe mfano (1x2)

h) Mfyeke nyasi yote! (1x1) (Tathimini majibu ya mwanafunzi)

i) – Mtoto alimnunulia mzazi wake mkate.
- Mtoto alinunua mkate kwa niaba ya mzazi wake.
- Mtoto alinunua mkate kutoka kwa mzazi wake.
- Mtu fulani pamoja na mzazi wake wote walipata mkate.

j) Alimpa/alimkabidhi
butu (1×2)

k) Nyenzo zikitumika magogo yatasonga haraka.

l) ja – ma – (jani – majani) (1/2 muudo)
ji – me - (jino – meno) (1/2 mfano)
0 - ma - gari - magari

m) i)Sentensi arifu / sentensi ya taarifa (1 x 1)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

ii) Sentensi ulizi/ maswali (1 x 1)

n) Maharusi walifunga ndoa baadaye / hatimaye / kisha /kisha / halafu walienda Afrika kusini kwa fungate. (2 x 1)

o) Kwa sababu ya kutotii kwao maisha ya mijini hayakuwaendea vibaya.

p) Uginjwa wa malaria hufisha watu wengi

q) S --------- KN+ KT

KN -------- N+V+S̄

N ----------Timu

V -------- yao

S̄ --------iliyotia fora sana

KT ------ T + E

T ------- ilituzwa

E ------ tena

r) yambiwa – mnuna wake

kiima – kijana hodari (1 x 2 )

s) yu- t kipungufu

anastahili – ts/Ts

kuachiliwa – T (kikuu)

t) Mwizi alishikwa alipotekeleza wizi.(kadiria jibu la mwanafunzi)

u) ubwege / upumbavu / uzumbukuku / ujahili

kiambo / kitongoji / kaya / karia / (½ x 2)

v) Cha kuzama hakina nahodha

La kuvunda halina ubani

Sikio la kufa halisikii dawa wala kafara

Ajali haina kinga ( 1x 1)

<u>ISIMU JAMII</u>

a) - Matumizi ya lugha shawishi

- Hali ya kuchanganya ndimi / kuhamisha ndimi
- Matumizi ya misamiati teule (MAJINA YA TAALUMA)
- Hali ya uradidi / urudiaji
- Kushirikisha maswali mafupi mafupi
- Matumizi ya lugha ya kitamathali – taswira /jazanda

(1x5)

b) <u>Sifa za sajili ya bungeni</u>

- Huwa na matumizi ya sentensi fupifupi / kauli fupifupi
- huwa na matumizi ya sentensi / kauli ndefu /maelezo marefu
- huwa na matumizi ya msamiati teule/ maalum,`spika'.
- Huwa na matumizi ya lugha ya heshima
- Huwa na matumizi ya hali ya kuchanganya mdimi / msimbo( hali ya kuhamisha ndimi)
- Huwa na hali ya kunukuu / kurejelea vitabu maaalum (katiba)
- Huwa na matumizi ya lugha amrishi ( 1x5)

<u>TB Sharti mwanafunzi atoe mfano wa sifa anazotoa</u>



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

½ kwa sifa
½ kwa mfano
(Adhibu makosa ya samihi na hijai)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes